

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## Jukwaa la Watumiaji Tanzania

Tanzania Consumer Forum (TCF)

### **HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. ALBERT JOHN CHALAMILA, MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM KWENYE MAADHIMISHO YA KILELE CHA SIKU YA HAKI ZA MTUMIAJI DUNIANI UKUMBI WA KARIMJEE, DAR ES SALAAM, TAREHE 15 MACHI, 2024.**

Waheshimiwa Makatibu Wakuu wote mliopo hapa,

Waheshimiwa Wakurugenzi Wakuu, Mamlaka za Udhhibiti (LATRA, EWURA, TCRA na TCAA),

Waheshimiwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ushauri ya Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa (LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC na TCAA CCC),

Waheshimiwa Makatibu Watendaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa ((LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC na TCAA CCC),

Waheshimiwa Wasajili Mabaraza ya Ushindani, FCT na ZFCT,

Mheshimiwa Mkurugenzi Mkuu, ZFCC,

Waheshimiwa Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi,

Waheshimiwa wageni waalikwa, Wanahabari Mabibi na Mabwana,

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Afya njema, na Baraka ya kukutana hapa kwa ajili ya siku hii adhimu ya kuadhimisha kilele cha Siku ya Haki za Mtumiaji Duniani, ambapo huadhimishwa kila mwaka, ifikapo tarehe 15 Machi.

### **Mabibi na Mabwana,**

Nimearifiwa na kusikia kwenye taarifa yenu kuwa, Jukwaa la Mtumiaji ni muunganiko wa hiari wa Taasisi zilizoanzishwa kwa Sheria za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Miongoni mwa taasisi hizo ni pamoja na LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC, TCAA CCC, ZFCT na ZFCC.

Ninapenda kuwapongeza wote kwa kufanikisha maadhimisho haya **Kitaifa hapa Jijini DAR ES SALAAM**, na hii inadhihirisha ushirikiano mkubwa, na wa kidugu, miongoni mwa taasisi zote zinazosimamia HAKI, MASLAHI na UWAJIBIKAJI wa mtumiaji wa huduma katika Taifa letu. Umoja na upendo wa namna hii, umekuwa ukihimizwa na kuongozwa vyema na viongozi wetu Wakuu wa Taifa letu, **Mh. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na **Mh. Dkt. Hussein Mwinyi**, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### **Mabibi na Mabwana,**

Kauli mbiu ya maadhimisho haya, inayosema **‘Akili Mnemba (Artificial Intelligence) inayozingatia Haki na Uwajibikaji kwa Mtumiaji’** ina akisi umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma. Pia kwa kutumia teknolojia hii inaendana moja kwa moja na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita, katika kuhamasisha matumizi ya Teknolojia ya Habari katika kuhudumia watumiaji katika sekta **za Maji, Nishati, Mawasiliano, Usafiri wa Anga na Usafiri Ardhini.**

Pia Ili Serikali iweze kufikia lengo namba tisa (09) la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (2030) linasisitiza Viwanda, Ubunifu na Miundombinu ambapo Akili Mnemba ni teknolojia ambayo inatumika katika kufanikisha azma hii.

### **Mabibi na Mabwana,**

Akili Mnemba, kama zilivyo teknolojia nyingine nyingi inakua kwa kasi kubwa duniani na hivyo nyanja na taasisi mbalimbali hazina budi kujiandaa kikamiifu ili kuipokea teknolojia

hii na kuifanya sehemu muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa huduma mbalimbali. Hii ni kwa sababu teknolojia hii inawawezesha watumiaji na watoa huduma kupata taarifa sahihi na kwa wakati (Real time information) ili kusaidia katika kufanya maamuzi ya kuboresha huduma mbalimbali kwa mtumiaji.

### **Mabibi na Mabwana,**

Ikumbukwe kwamba mtumiaji wa huduma ana haki mbalimbali zikiwemo haki ya:

- (a) Usalama;
- (b) Kupewa taarifa;
- (c) Kuchagua;
- (d) Kusikilizwa;
- (e) Kuelimishwa;
- (f) Kupata mahitaji muhimu;
- (g) Kulipwa fidia; na
- (h) Kutunza mazingira.

### **Mabibi na Mabwana,**

Ninapenda kuwapongeza wadau wote mliopo hapa na taasisi zilizoshiriki maadhimisho haya, pia ushiriki wenu katika Mdahalo huu muhimu ambapo wadau mbalimbali pamoja na mambo mengine wanategemewa kuwasilisha taarifa, maoni, kero, uzoefu pamoja na changamoto ambazo zinaweza kutarajiwa kuambatana na matumizi ya Akili Mnemba na njia mbadala za kukabiliana nazo.

### **Mabibi na Mabwana,**

Ni dhamira na ahadi ya Serikali ya awamu ya Sita kuendelea kujikita katika maboresho na matumizi ya teknolojia ili kuendelea kuwezesha huduma bora kwa watumiaji ili waendelee kuwa na Imani na Serikali yao.

### **Ndg, Mabibi na Mabwana,**

Sasa napenda kutamka kuwa nimefungua rasmi Mdahalo wa Siku ya kilele cha maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Haki za Mtumiaji Duniani kwa mwaka huu 2024, yaliyofanyika hapa Dar es Salaam.

**Ninawataka wote kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu, Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

**MUHIMU:** Taasisi zinazounda Jukwaa la Watumiaji Tanzania (TCF) ni:

LATRA CCC	:	LATRA Consumer Consultative Council
EWURA CCC	:	EWURA Consumer Consultative Council
TCRA CCC	:	TCRA Consumer Consultative Council
TCAA CCC	:	TCAA Consumer Consultative Council
ZFCT	:	Zanzibar Fair Competition Tribunal
ZFCC	:	Zanzibar Fair Competition Commission

